SHUGHULI ZA KISWAHILI UFAHAMU - CBC GRADE 2 TERM 1 EXAMS 2023

Ufahamu (Alama 10)
Soma hadithi kisha ujibu maswali yanayofuata. (Alama 5)

Imani akiamka asubuhi, ananawa uso. Anapiga meno mswaki kwa kutumia mswaki na dawa ya meno. Yeye huoga kabla ya kunywa kiamsha kinywa. Anatumia kikata kucha kukata kucha zake. Imani hutumia kichana kuchana nywele zake. Imani anapenda kuwa safi kila siku. Anajua usafi huleta afya bora.

a. Taja mambo mawili anayofanya Imani anapoamka. (alama 2)
b. Imani akitaka kukata kucha, atatumia nini?
c. Kwa nini Imani anapenda kuwa safi kila siku?
d. Tunatumia.....kuchana nywele zetu.

Soma hadithi kisha ujibu maswali yanayofuata.(Alama 5)
Mama yangu ni mkulima. Yeye hupanda mimea tofauti kama vile mihindi, miharagwe, mboga na migomba. Yeye pia anafuga wanyama wa nyumbani kama vile ng'ombe, punda, mbuzi na sungura. Ng'ombe hutupa maziwa. Sisi hunywa maziwa kila siku.
Pia tunatumia maziwa hayo kupika chai na kutengeneza sharubati. Kwa kweli mama yangu ni hodari.

a. Taja mimea miwili ambayo mama amepanda. (alama 2)
b. Ni mnyama yupi anatupa maziwa?
c. Taja matumizi mawili ya maziwa. (alama 2)
    i. .....
    ii. .....

2.. SARUFI (Alama 15)

1. Unda maneno matatu ya sauti 'd' (Alama 3)
    a. .....
    b. .....
    c. .....
2. Jaza pengo: (alama 2)
    a. g __ __ rid ___
    b. n__iz__